

JIBU: Ubarikiwe ndugu...Mlozi ni mti fulani, unaositawi sana sana huko mashariki ya kati (Lebanoni, Israeli, Palestina n.k.).Jina lake kwa kiyahudi unaitwa “**SHAKEI**” na tafsiri yake ni

KUTAZAMA/KUANGALIA...Kwahiyo Yeremia kuonyeshwa pale Mti wa Mlozi ni lugha tu ya picha anayoonyesha kwamba Bwana ANATAZAMA, na je! anatazama nini?..Anatazama NENO lake ili alitimize alilolinena juu ya Israeli..na ndio maana ukisoma hapo anasema..

Yeremia 1: 11 Tena neno la Bwana likanijia, kusema, Yeremia, waona nini? Nikasema, Naona ufito wa mlozi. 12 Ndipo Bwana akaniambia, Umeona vema, kwa maana ninaliangalia neno langu, ili nilitimize...

Kumbuka pia Mungu huwa anatazama Neno lake ili alitimize kwa namna zote, Hivyo kama ni jema, ni lazima alitimize, na kama ni baya juu ya watu wake ni lazima alitimize pia!.Kote kote. Lakini tunaona Israeli walikuwa waasi kwa Mungu tangu zamani, ukisoma katika habari za wafalme utaona jambo hilo, jinsi walivyokuwa wanamuasi Mungu mpaka akawaapia kuwa wataenda utumwani tena Babeli, kwa vinywa vya manabii wake waliotangulia kabla ya Yeremia mfano Isaya n.k. Na ndio maana hapo Yeremia anaonyeshwa kama **UFITO(FIMBO)** tu, ya mlozi, Ikimaanisha kuwa Mungu analitazama NENO lake, na kulitimiza juu yao

kama ADHABU na sio **BARAKA...**

kwasababu FIMBO ni kwaajili ya kuadhibu siku zote tunajua hilo. Hivyo Ukizidi kuendelea mistari inayofuata ndio utaona mabaya yote Mungu aliyoyanena juu ya yao yalikuja kutimia ikiwemo kuchukuliwa utamwani Babeli.

ubarikiwe

Mada Nyinginezo:

FIMBO YA HARUNI!

UFUNUO: MLANGO WA 1

**SANDUKU LA AGANO LILIKUWA LINAWAKILISHA NINI KATIKA
AGANO JIPYA?**

**NI RAHISI KWA NGAMIA KUPENYA KATIKA TUNDU LA
SINDANO, JE! NI SINDANO IPI HIYO INAYOZUNGUMZIWA?**

Mti wa MLOZI alioonyeshwa nabii Yereimia 1:12 tafsiri yake ni nini?

SWALI LA KUJIULIZA!

RACA

AMIN! NAWAAMBIA KIZAZI HIKI HAKITAPITA

USIPIGE MATEKE MCHOKOO!

Rudi Nyumbani:

Share on:
WhatsApp